MWONGOZO

# SHULE YA UPILI YA SUNSHINE

**KARATASI YA 102/2**
**KISWAHILI**
**KIDATO CHA PILI**
**MACHI 2014**
**MUDA: SAA MBILI**

**JINA:……………………………………………………NAMBARI YA USAJILI:…………**

**DARASA: …………………..TAREHE:………………**

**Maagizo:**
1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C and D.
2. Jibu maswali yote katika karatasi hii kwenye nafasi zilizoachwa.
3. Makosa yote ya sarufi na hijai yataadhibiwa.

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| SEHEMU | MADA | UPEO | TUZO |
|---|---|---|---|
| A. | UFAHAMU | 15 | |
| B. | SARUFI | 40 | |
| C. | ISIMU JAMII | 10 | |
| D. | FASIHI SIMULIZI | 15 | |
| | JUMLA | 80 | |

**Soma taarifa ifuatayo kisha jibu maswali yafuatayo (Al. 15)**

Wanawake, wanaoishi katika maeneo ya mashambani katika nchi zinazoenedelea ni baadhi ya watu waliotopea na kubobea katika uchochole mkubwa. Jumla ya idadi kubwa ya wanawake hawa wanaoishi chini ya kiwango cha chini cha umaskini inakadiriwa kuwa zaidi ya million 600. Hii ni idadi kubwa hasa ikikumbukwa kuwa ni asilimia kubwa ya wanawake wanaoishi kwenye maeneo haya.

Ulimwengu umeshuhudia ongezeko kubwa la idadi ya watu pamoja na kuwako kwa matatizo ya kiuchumi duniani. Kadhalika matatizo mengine na mitafuruku na vita vya kikabila, majanga ya kiasili mathalani mafuriko, ukame , milipuko ya volkano n.k. Usisahau pia kuwa kuna uharibifu wa kimazingira, mabadiliko ya desturi na kusambaratika kwa familia na misingi yake. Tatizo lingine ni kuwa kuna kuongezeka kwa hali ya wanawake kuwa wazazi pekee na hivyo kuongeza familia. zinazosimamiwa na wanawake (ambao tumewataja kuwa wanakumbwa na umaskini mkubwa.)

Wanawake wanaoishi mashambani wanakumbwa na makubwa. Kwanza, kama maskini wanaiishi katika mazingira magumu. Vile vile kama wanawake wanakabiliana na mapendeleo ya kisera na kitamaduni yanayowadharau na kuwapuuza wanawake na mchango wao katika maendeleo. Tatu, kama viongozi wa familia, hasa wanaolea na kutunza jamaa za mzazi mmoja, wanapambana na uongozi wa familia pamoja na uzalishaji. Aghalabu hawapati usaidizi wowote katika majukumu kama haya bali wanalazimika kupambana nayo peke yao. Kutokana na hayo yote wanawake hawapati nafasi nzuri kushiriki katika maamuzi ya maswala yanayowahusu. Maswala mengi yanaamuliwa na wanaume pasipo kuwahusisha wanawake.

Licha ya dhiki yao kubwa, wanawake hawa wanachangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa njia mbali mbali. Mchango huu unaonekana katika kiwango cha jamii , taifa na familia. Katika kiwango cha kijamii na kitaifa wanawake ndio chanzo cha nguvukazi kwani ni wao na watoto wao wanaotekeleza kazi nyingi hasa za nyumbani na mashambani. Mara nyingi huwa na uwezo bora wa kutunza chochote walicho nacho kuliko wenzao wanaume.

Kifamilia wanawake wa mashambani wanashugulika mchana kutwa katika hali ngumu ya hewa aidha jua kali au mvua huku wameeleka wanao migongoni wakilima mashamba ili kupata chakula kwa familia zao. Jukumu la kuandaa chakula nyumbani bado linaachiwa wale wale wanawake wanaokizalisha mashambani.

Jambo lisilopingika ni kwamba wanawake wanatekeleza majukumu makubwa na muhimu katika kizazi cha binadamu na ndio hasa mihimili ya jamii yoyote staarabu. Kwa hivyo, ni kinaya kitupu kudhalilisha wanawake. Mataifa mengi yaliyoendelea ni yale yaliyoondoa vikwazo vyote mbele ya wanawake na kuwaacha watekeleze wajibu wao. Kadhalika wanaume wa huko wanawaona wanawake kuwa wenzao katika kujenga jamii wala sio watumwa au watumuishi wao wanaoumia na kutumikishwa kama vifaa na bidhaa. Inafaa jamii zinzodunisha wanawake zitambue kuwa ubaya wa tendo hili sio tu kudumaza maendeleo yake bali pia kutoa mfano mbaya kwa vijana ambao wataendeleza ukandamizaji huu kwa vizazi vijavyo. Kwa hivyo, jamii inawabijika kutenda lilio sawa kwa kuwapa hadhi wanawake wote.

***Maswali***

(a)Ipe taarifa hii anwani mwafaka (Al. 1) WANAWAKE WA MASHAMBANI

(b) Nakili maafa <u>matatu</u> ya kimaumbile yaliyotajwa katika kifungu hiki. (Al. 3)

Mafuriko
Ukame
Milipuko ya Volkano (3×1)

(c) Eleza sababu <u>tatu</u> zinazowazuia wanawake kushiriki katika maamuzi ya masuala yanayowahusu kulingana na makala haya.(Al. 3)

(i) Umaskini
(ii) Mapendeleo ya kisera na kitamaduni
(iii) Ulezi wa kifamilia pamoja na uzalishaji

(d) Wanawake hutekeleza majukumu gani katika jamii na taifa kutokana na makala haya?(Al.3)

(i) Nguvukazi – nyumbani na mashambani – kuzalisha mali.
(ii) Hutunza mali ya jamii
(iii) Kuandalia familia chakula

(e) Kuna tofauti gani baina ya wanawake wa mataifa yaliyoendelea na yale ambayo hayajastawi. (Al. 2)

– Mataifa yaliyoendelea yameunda vikundi vingi mbele ya wanawake na kuwaacha watekeleze wajibu wao. Na mataifa ambayo hayajastawi bado vikundi vipo.
– ~~Wanawake wa nchi~~ zilizoendelea huwaona kama wenzao ilhali wa mataifa yasiyostawi wanawake ni watumwa au watumishi wao

(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye taarifa. (Al. 3)

i) Uchochole

Ukata / ufukara / umaskini

ii) Kudhalilisha

Fanya mtu kuwa mnyonge / Fanya mtu kuwa duni

iii) mitafuruku

Ghasia, wasiwasi na kutokuelewana.

## SARUFI YA MATUMIZI YA LUGHA

1. Taja sifa mbili bainifu za irabu /o/. (al 2)

   Irabu viringwa / Hutamkwa midomo ikiwa imeviringwa.
   Irabu ya nyuma / Hutamkwa nyuma ya ulimi
   Hutamkwa ~~nyuma~~ ulimi ukiwa umeinuliwa juu-wastani (Zozote 2x1=2)

2. Tambua aina ya vitenzi. Mwanafunzi ambaye ni mcheshi angali analia. (al 3)

   ni – Kishirikishi kipungufu ✓ ½
   angali – Kisaidizi ✓ ½
   analia – Kikuu ✓ ½

   angali analia – Sambamba
   zozote (3x1) = 3

3. Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi huru cha nafsi ya kwanza wingi. (al 2)

   Sisi tunaimba vizuri (Apigie mstari kiwakilishi ( a siyo atuzwe 0)

4. Ainisha viambishi katika sentensi ~~na viambishi kivyo~~. (al 3)

   Aliyepigiwa

| A | li | ye | pig | iw | a |
|---|---|---|---|---|---|
| nafsi ya tatu wingi | wakati uliopita | -o- rejeshi | mzizi | kauli ya kutendewa | kiishio |

5. Andika neno moja lenye mpangilio ufuatao wa silabi. KKI. (al 1)

   Njama (Apigie mstari silabi,) ~~la siyo~~

6. Andika kwa wingi. (al 3)

   Kuku ambaye alinunuliwa na mama ametaga yai. ½

   Kuku ½ ambao ½ walinunuliwa na akina mama ½ wametaga ½ mayai ½

7. Tunga sentensi sahihi kwa kutumia kinyume cha neno <u>cheka.</u> (al 1)

   Anapenda kulia sana. ✓ 01

8. Mofimu ni nini? (al 2)

   Mofimu ni kipashio kidogo cha lugha chenye maana ambacho hakiwezi kugawika zaidi bila kupoteza maana yake. (Jibu lingine sahihi)

9. Kanusha sentesi hii. (al 1)

Wandera huvua samaki. ✓ 01

Wanderi havui samaki

10. Tambua aina ya nomino na ueleze ni za aina gani. (al 3)

Okubasu ni mwanafunzi mwenye upendo sana.

Okubasu – pekee/mahususi
Mwanafunzi – kawaida
Upendo – dhahania.

11. Maneno haya ni ya ngeli gani? (al 2)

Konokono – A-WA
Chama – KI-VI
Manukato – YA-YA
Uovu – U-YA

Kila kitahiniwe atuzwe ½

12. Eleza matumizi mawili ya nukta pacha. ~~(al 3)~~ alam 2

(a) Kuorodhesha
(b) Dayolojia, mazungumzo au tamthilia
(c) Kutenganisha saa na dakika. (zozote 2x1 = 2)

13. Kamilisha sentensi kwa kutumia '-ote' (al 1)

Pote pamechafuka sana. ✓ 1

14. Pigia mstari vihusishi katika sentensi hizi. (al 3) 01

Abeid amejificha ndani ya nyumba ✓ 01

Ameomboleza tangu jana jioni ✓ 01

Alikaa chini ya mti ✓

(Kila kitahiniwa alama 01)

15. Tambua kundi nomino na kundi tenzi katika sentensi hii. (al 2)

Mtoto mvulana angali anacheza uwanjani.
KN KT

16. Andika kwa ukubwa, (al 3)

Ng'ombe huyu amemsumbua ~~motto~~ mtoto yule aliyekuwa akisoma kitabu.

Gombe hili limekisumbua kitoto kile kilichokuwa kikisoma kijitabu. [Sentensi lazima iwe sahihi]

17. Kamilisha jedwali hili. (al 4)

| Kauli ya kutenda | Kutendwa | Kutendeka |
|---|---|---|
| Funga | Fungwa | Fungika |
| Chota | Chotwa | Choteka |
| Tenda | Tendwa | Tendeka |
| Koroga | korogwa | Korogeka |

[Kila kitahiniwa ½ alama]

18. Tunga sentensi moja kwa kutumia maneno haya. (al 2)
(i) Mbao
(ii) Bao

Matuko Heje alipewa mbao baada ya kufunga bao zuri wakati wa mechi yao.

~~Senten~~ (Atumie maneno haya Nzuri)

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

**Maagizo: Jibu maswali yote.**

1. Isimu jamii ni nini? (al 2)

Taaluma ambayo hushughulikia uhusiano uliopo baina ya lugha na jamii.

2. **Bungo:** Kumbe uliruka mwala vizuri. Haleluya!
**Kali:** Nimneroll poa! Hakuna diambo. Wewe?
**Bungo:** Namshukuru subhana.
**Kali:** Mazee, hata mahewa ya leo yamenijazz!

(a) Mazungumuzo haya yanatokea mahali gani? Eleza jibu lako. (al 2)

Mazingira ya kuabudu (kanisani) - kuna msamiati unaohusishwa na ibaada. Mfano Haleluya, Namshukuru subhana ambao hutumiwa katika mazingira ya kanisa.

(b) Eleza sifa za lugha inayotumiwa na wazungumzaji. (al 2)

1. lugha ya mseto : ~~Kiingereza~~, Kiswahili na sheng
2. lugha iliyo na msamiati wa seli ya Kiwabudu. Mf. Ndelele
3.) Matumizi ya misemo Mf. diambo (Zozote 2)

3. Fafanua sifa mbili za sajili ya maabadani. (al 2)

1. Huwa na msamiati maalum. Mf. sadaka, dhambi
2. Kuna urejeleaji wa maandishi matakatifu. Mf. Biblia, Kurani
3. Urudiaji wa maneno. Mf. Amina Amina.
4. Matumizi ya viziada lugha Mf. ishara kusisitiza jambo (Zozote 2)

4. **Siki:** Unamwonaje?
**Waridi:** Kitoto chenyewe kiriba chaongoza.
**Siki:** Tatizo la … utapiamlo lipo.
**Waridi:** Mpaka sasa wapo watu wasioelewa umuhimu wa lishe bora?
**Siki:** Waridi ni halio ya maisha. Mwandalie mchanganyiko wa sukari na chumvi katika maji moto. Huenda itasaidia apate nafuu.

(a) Hii ni sajili gani? (al 1)

Sajili ya hospitalini au Zahanatini.

(b) Toa sifa moja ya sajili uliotaja. (al 1)

1. Msamiati maalum : Utapiamlo
2. lugha ya kuhoji / kudadisi.

(Yoyote 1)

**FASIHI SIMULIZI (ALAMA 15)**

1. Tofautisha kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi ukizingatia vigezo hivi: (al 2)

(a) Hadhira F.S. – Hai : Huonana ana kwa ana na Mtambaji
F.A. – Si hai. Msomaji huona tu yaliyo vitabuni bila kuonana ana kwa ana na Mwandishi

(b) Mabadiliko F. Simulizi – Msimulizi anaweza kubadilisha/kubadilisha uwasilishaji wa utanzu fulani kutegemea hadhira
F. Andishi – Ni Mwandishi aliye na uwezo wa kubadilisha kazi yake. Msomaji hawezi kamwe.

1

2. Eleza mambo mawili yanayochangia kubadilika kwa fasihi simulizi. (al 2)

(i) Hadhira yake – Kwa Watoto, Watu wazima
(ii) Wakati – Hutegemea Matukio katika jamii.
(iii) Fanani – Mtindo wake wa kusimulia kazi
(iv) Maendeleo katika Maisha ya Binadamu – Kwa Sayansi & Teknolojia
(v) Mazingira – ya Jamii Mbalimbali

3. Taja na ufafanue aina mbili za hadhira katika fasihi simulizi. (al 2)

Hadhira Tuli – Haichangii / Hawashiriki katika uwasilishaji

Hadhira Tendi – Huchangia katika uwasilishaji

4. Kuna umuhimu gani wa kufunza fasihi simulizi shuleni? Toa hoja tatu. (al 3)

(i) Hukuza uwezo wa kufikiri na kudadisi – vitendawili, Mafumbo,
(ii) Hukuza Lugha ya wanafunzi – Ulumbi, Malumbano ya utani
(iii) Hukuza Ubunifu wao – Hadithi, nyimbo, Mashairi
(iv) Hutoa Maadili Muhimu – Methali, Mawaidha, nyimbo

5. Fafanua sifa tatu za ngano. (al 3)

– Fomyula ya Ufunguzi na kimalizio
– Hadithi hizi ni za kimapokeo – Hurithishwa vizazi hadi vingine.
– Matumizi ya mbinu ya urudiaji kwa wingi – Maneno, vifungu, sauti
– Wahusika – Binadamu, Wanyama, Wazimwi, Mizimu, Miungu n.k.
– Matumizi ya nyimbo – kituliza kwa hadhira.
– Ploti sahili – Fantasia – Zina Mafunzo kwa wanajamii.

6. Tofautisha kati ya visakale na mighani. (al 2)

Visakale – Masimulizi kuhusu visa vilivyotokea hapo zamani katika jamii

Mighani – Ni hadithi za Mashujaa wanaoaminika kuwa waliishi katika jamii na walitenda Matendo yasiyo ya kawaida

7. Methali ni nini? (al 1)

Ni semi fupifupi za kimapokeo zenye kueleza fikra, maarifa, hekima na Mafunzo yanayotokana na uzoefu wa jamii Mahususi.